# Maelezo ya Msingi kwa Wazazi

Kama mzazi wa mwanafunzi ambaye huenda anapokea elimu maalumu, huenda una haki fulani ambazo zimehakikishwa na sheria ya serikali kuu iitwayo Sheria ya Watu wenye Ulemavu (IDEA). Sheria hii inafafunua mchakato ambao unahakikisha kwamba una fursa na haki ya kuhusishwa kama mwanachama sawa ambaye anafanya maamuzi kuhusu mtoto wako.

Mojawapo ya haki zako ni kufahamishwa (kimaandishi, katika lugha yako ya mwanzo) kuhusu taratibu za kujilinda (haki za kisheria) ambazo zipo kwa ajili yako. Nakala za haki hizi lazima shule ikupatie katika sehemu fulani ya mchakato. Ikiwa ungependa kufahamu zaidi kuhusu haki zako au jinsi unaweza kuwa mshirika wa mzuri wa shule, tafadhali wasiliana na Utah Parent Center kwenye 801-272-1051 au tutembelee kwenye tovuti ya www.utahparentcenter.org

## Elimu Maalumu ni Nini?

Imenukuliwa moja kwa moja kutoka IDEA

**'Elimu Maalumu'** inamaanisha mafundisho yaliyoundwa mahususi, bila malipo kwa wazazi, ili kufikia hitaji maalumu la mtoto mwenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya darasani, mafunzo ya viungo vya mwili, mafundisho ya nyumbani, na mafunzo katika hospitali na taasisi.

Neno hili linajumuisha mafunzo ya matamshi, au huduma zinazohusiana...

Neno hili aidha linamaanisha **mafunzo ya kiufundi** kama inajumuisha mafundisho yaliyoundwa kwa njia mahususi, bila kuwalipisha wazazi, kufikia mahitaji maalumu ya mtoto mwenye ulemavu.

**'Huduma Zinazohusiana'** zinamaanisha usafiri na huduma zinasaidia ukuaji, urekebishaji na huduma-saidizi nyinginezo (ikiwa ni pamoja na mafunzo ya matamshi na huduma za masikio, huduma za kisaikolojia, za mwili na utendaji, burudani, ikiwa ni pamoja na burudani ya kimatibabu, kazi ya huduma ya kijamii, huduma za ushauri nasaha, pamoja na ushauri wa kukarabati, uzoeshaji na huduma za usogezaji, na huduma za afya, ila huduma za afya zitakuwa kwa ajili ya kupimwa na kutathminiwa tu) jinsi itakavyohitajika ili kusaidia mtoto mwenye ulemavu kunufaika kutokana elimu maalumu, na inajumuisha utambuaji wa mapema na kutathmini mazingira yanayoleta ulemavu katika watoto.

## Muhtasari wa Mchakato wa Elimu Maalumu

Mchakato wa elimu maalumu umeundwa kuhakikisha kila mtoto mwenye ulemavu atapata elimu ambayo inamlenga yeye binafsi ili kufikia mahitaji yake. IEP (Programu ya Elimu Inayomlenga Mtoto) ni mpango inayoundwa na timu ya IEP. Wewe kama mzazi ni sehemu ya timu inayofanya maamuzi programu ya mwanafunzi.

Ni muhimu kwa wazazi kuwa washirika wa hakika katika mchakato wa kufikia maamuzi ya kuhusu watoto wao. Taarifa ambazo mzazi anaweza kushiriki ni muhimu sana kwa shule.

Ni muhimu pia kwa mzazi kuelewa na kuheshimu maoni ya wafanyikazi wa shule. Kwa kuingiliana kwa njia ya heshima baina na kufanya kazi pamoja, wazazi na wafanyikazi wa shule wanaweza kuunda programu inayofaa na nzuri kwa mtoto.

## Kupatikana kwa Mtoto/Rufaa

Wilaya ya shule lazima iwe na utaratibu wa kupata watoto wenye ulemavu. Mzazi au mfanyikazi wa shule anaweza kutuma mtoto kutathminiwa ili kubaini kama huduma za elimu maalumu zinahitajika. Wazazi wanaweza kutuma ombi maalumu kwa Idara ya Elimu Maalumu ya shule. Matokeo ya rufaa hii yanaweza kuwa:

- Shule kufanya tathmini kamilifu.
- Shule itaamua kwamba tathmini haihitajiki.

## Tathmini (Upimaji)

Tathmini ili maamuzi yafanyike kama mtoto anafaa elimu maalumu ni mchakato wa kukusanya habari kuhusu mtoto ambayo itatumiwa kuuamua kama mtoto anafaa kupewa huduma na ni katika kategoria gani ya ulemavu mtoto anafaa kuhudumiwa kwayo. Habari hii pia husaidia kuamua uwezo na mahitaji ya mtoto ambavyo vitazingatiwa katika kuamua juu ya huduma na mahitaji ya mtoto. Lazima wazazi watoe ruhusa ya ili tathmini ifanyike.

Tathmini lazima iwe ya kufaa kwa mtoto na izingatie mambo kadhaa aliyoorodheshwa kisheria. Wazazi watakuwa na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika IEP kama wanaelewa matokeo ya tathmini. Kama wazazi hawakubaliani na matokeo ya tathmini,wanaweza kuomba kupata tathmini huru (upimwaji utakaofanywa na mtu nje ya shule) kwa gharama ya wilaya ya shule kwa kufuata mwongozo fulani.

Baadhi ya watoto ambao hatafaulu kuwekwa katika elimu maalumu wanaweza kuwa na sifa za huduma chini ya Sehemu 504 ya Sheria ya Ukarabati ya 1973 ambayo inalinda hali za watu wenye ulemavu Mpango wa Sehemu ya 504 unapangwa na timu ambayo inajumuisha wazazi na inayoweza kumpa mwanafunzi vifaa au huduma zinazohitajika.

## Sifa Zinazohitajika (Uainishaji)

Timu (ikiwa ni pamoja na wazazi) inahakiki takwimu zinatokana na tathmini na kuamua kama mtoto ana sifa za kuwekwa katika mojawapo ya kategoria za elimu maalumu. Vigezo vinavyohitajika katika kila kategoria vinaamuliwa na sheria ya nchi au jimbo.

## Mkutano wa IEP

Timu (wakiwemo wazazi) hukutana kuunda programu faavu ya kumhudumia mtoto. Katika mkutano wa timu, mahitaji ya kielimu ya mtoto hujadiliwa. Malengo yanayopimika ya mwaka na malengo ya muda mfupi yaliyokubaliwa na wote. Kwa msingi wa malengo, maamuzi yanafanywa kuhusu jinsi mahitaji ya kielimu ya mtoto yatafikiwa, ikiwa ni pamoja na elimu maalumu na huduma zinazohusiana na usaidizi wa ziada na huduma vitakavyotolewa. Vipengele vingine vinavyohusiana na elimu ya mtoto lazima vizingatiwe. IEP inatenga mapema kwa njia ya maandishi rasilimali zinazohitajika kumhudumia mtoto huyo. IEP aidha inatumika kama kifaa cha tathmini na inaweza kubadilishwa wakati wowote, au timu inaweza kukutana wakati wowote.

## Mpito

Kabla ya mtoto kupita miaka 14, lazima timu ijumuishe maelezo kuhusu huduma za mpito zitakazohitajika kumsaidia mwanafunzi kuvuka kutoka shuleni hadi shughuli za baada ya maisha ya shuleni. Lazima huduma za mpito zitolewe kuanzia kufikia miaka kumi na sita.

## Kuwekwa Anakofaa

Timu (ikijumuisha wazazi) huamua anakofaa kuwekwa mtoto kwa mujibu wa programu waliokubaliana katika mkutano wa IEP. Timu huuliza, "Ni wapi huduma hizi zinaweza kutolewa?" Mwanafunzi anafaa kuhudumiwa katika Mazingira Yasiyokwanza Sana (LRE) yanavyofaa kwa huyo mtoto

## Uhakiki wa Kila Mwaka



Timu (wakiwemo wazazi) hukutana angalau mara moja kwa mwaka ili kutathmini programu nzima ya mtoto na kusasisha IEP. Ikiwa itabainika kwamba mtoto sasa hana sifa za kupewa elimu maalum, mtoto hataendelea na mchakato na IEP na hataondoka kwenye programu.

## Haki za Kufuata Utaratibu

Una haki ya kutofautiana na timu wakati wowote katika cha mchakato. Kama utatofautiana, una haki za kufuata utaratibu (kisheria), ikiwemo upatanishi, ambavyo vimefafanuliwa katika sheia. Haki hizi zimeelezwa kwa kina katika nakala yako ya hati ya haki za mzazi ambayo unapewa na shule.

Huu ni muhtasari wa msingi tu juu ya mchakato wa elimu maalumu, na hauna haki zako zote. Kwa maelezo zaidi kuhusu Mchakato wa IEP, tafadhali tembelea tovuti ya www.utahparentcenter.org. Hapo utaona Video ya Mafunzo ya 'Wazazi kama Washirika katika Mchakato wa IEP' Au pakua 'Wazazi kama Washirika katika Mchakato wa IEP - Kijitabu cha Mzazi'.

## Kama unahitaji usaidizi...

Kama una mashaka au maswali au unataka kujua maelezo kwa kina kuhusu haki na majukumu yako, unafaa kuuliza idara ya elimu maalumu katika shule ya mtoto wako. Kama una matatizo ambayo huwezi kusuluhisha na shule, unaweza kuita idara ya elimu maalumu ya wilaya yako ya shule. (Aidha unaweza kuwasiliana na shule yako au mratibu wa Sehemu ya 504 wa wilaya kwa usaidizi maswali au mashaka ya Sehemu ya 504.)

## Utah Parent Center

Kwa miaka 31, wafanyikazi wa Utah Parent Center wamesaidia kubadilisha maisha ya watoto wenye ulemavu. Sisi ni wazazi tunaowapa wazazi wengine usaidizi. Tunaelewa jinsi ilivyo na jinsi inavyohisi kuwa na mtoto mwenye ulemavu. Tumewahi kukivaa kiatu chako. Tumelia machozi ya furaha na ya kukatishwa tamaa, na tuko hapa kukusaidia kufaulu. Kwa kutoa warsha za bure, usaidizi wa mtu binafsi na maelezo ya kina kwa Kiingereza na Kihispania kote katika Jimbo la Utah – tunasaidia familia na watoto wenye mahitaji maalumu – kupata usaidizi wanaohitaji.